Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili –00005809 Toleo 3: Septemba, 2011

"Utetezi wa Sera na Utawala Bora Katika Sekta ya Afya"

Utangulizi

Na Victoria Amandus

MPENDWA msomaji karibu katika toleo la tatu la jarida la Sikika lenye lengo la kukufahamisha shughuli zilizotekelezwa ndani na nje ya shirika letu, dhumuni kubwa likiwa ni kuboresha huduma za afya nchini. Kwa kipindi hiki cha robo ya tatu ya mwaka Shirika lilifanikiwa kufanya utafiti wa awali katika mkoa wa Dodoma hususan wilaya za Kondoa na Mpwapwa. Katika kipindi hiki watanzania tulishuhudia midahalo mbalimbali ikifanyika katika kujadili mustakabali wa marekebisho ya katiba ya nchi. Ni matumaini yetu msomaji wetu utafurahia makala zetu katika jarida hili ili upate kufahamu nini kilijiri ndani na nje ya Shirika.

Shirika katika utekelezaji wake wa mpango kazi wa mwaka tulifanya tafiti za awali katika mkoa wa Dodoma katika wilaya za Kondoa na Mpwapwa. Lengo la tafiti hizi ni kutaka kufahamu kwa undani matatizo mbalimbali yanayokabili vituo vya afya. Matokeo ya awali ya utafiti yanaonyesha kuwa kuna upungufu mkubwa wa wahudumu wa afya unaosababishwa na mazingira magumu ya kufanya kazi, upungufu wa vifaa vya maabara kama vile mashine za CD4 kwa ajili ya kupimia CD4 kwa watu washio na virusi vya UKIMWI na pia ukosefu wa madawa muhimu pamoja na vifaa tiba katika vituo vya afya. Sikika itayatumia matokeo haya ya utafiti kwa kufanya ushawishi na utetezi kwa wahusika ili kuboresha huduma hizo hasa katika maeneo ya vijijini.

Katika kipindi cha mwezi (Julai – Semptemba) tulishuhudia wadau mbalimbali yakiwemo mashirika mbalimbali yalivyoandaa midahalo ya kujadili mabadiliko ya katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Majadiliano hayo yalivuta hisia tofauti kwa watu wengi wa rika mbalimbali huku kiu kubwa ikiwa ni kutaka kujua hasa ni nani anahusika na uteuzi wa tume huru ya kuratibu mchakato wa zoezi hilo. Wabunge wa Jamhuri wa Muungano hususan wale wa kambi rasmi ya upinzani walipinga kupitishwa mswada huu wakidai kuwa una mapungufu mengi ambayo kama rais atapitisha basi katiba yetu itakuwa bado na mapungufu mengi. Ili kuhakisha kwamba mambo yanayohusu afya yanaingizwa katika katiba

Baadhi ya wananchi wakipata maelezo ya mrejesho wa utafiti juu ya upatikanaji wa huduma bora za afya VVU/UKIMWI katika wilaya ya Mpwapwa.Utafiti huo ulifanyika mwaka jana na Shirika la Sikika.

mpya, wadau wa asasi zisizo za kiserikali na jumuiya za kiraia hapa nchini nazo hazikuwa nyuma kwani ziliunda muungano wao kwa jina la Jukwaa la Katiba ili ziweze kufikisha maoni yao katika vyombo husika. Sikika kama mdau muhimu katika masuala yenye maslahi kwa nchi Shirika pia ilishiriki kikamilifu katika mchakato huo wa mabadiliko ya katiba mpya. Shirika pia lilishirika katika maandalizi ya siku ya Sera ya Afya (Health Policy Day) iliyoandaliwa na Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya. Ushiriki wa Sikika ulijidhihirisha dhahiri katika vikundi kazi vya wizara ya afya (Technical Working Group) na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Regional and District Working Group) kwa lengo la kuwasilisha vipaumbele vinavyotokana na mapungufu yaliyoibuliwa kwenye tafiti mbalimbali zilizofanywa ili viweze kuingizwa katika mpango kazi wa Wizara ya Afya kwa mwaka 2012.

Pia, tulipata fursa ya kushirika katika ziara rasmi iliyoandaliwa na Wizara ya afya kwa lengo la kuangalia jinsi miradi yake ilivyotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2011. Ziara hiyo ilijumuisha wafadhili mbalimbali wa wizara ya afya na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayofanya kazi katika sekta ya afya. Ziara hiyo pia ilifanyika katika mikoa ya Manyara na Singida. Fursa hii ilikuwa ya pekee kwa Sikika kwani tulijifunza mambo mbalimbali na kupata picha halisi ya hali ya utoaji wa huduma za afya katika mikoa hiyo ambayo Sikika itaanza kufanya kazi mwaka 2012.

Kwa kipindi hiki Sikika ilifanikiwa kutumia mitandao yake ya *Twitter*, *Facebook* na *blog* katika kuibua na

NDANI

Mgawanyo mbovu wa bajeti: Kikwazo katika utoaji wa huduma bora za afya..... 2
Wananchi wanapaswa kudai haki ya afya katika katiba ijayo ya Tanzania..... 3
Motisha ni njia sahihi ya kuboresha huduma za afya nchini..... 4

kukuza mijadala mbalimbali inayohusu mapungufu na namna ya kufanya maboresho katika sekta ya afya. Lengo likiwa jinsi gani tunaweza kushirikiana kwa pamoja ili kuweze kuboresha huduma bora za afya katika vituo vyetu vya huduma na mfumo mzima wa utoaji na usambazaji dawa na vifaa tiba wa huduma za afya nchini.

Kwa taarifa zaidi usisite kutembelea tovuti ya Shirika www.sikika.or.tz na kwa maoni yoyote tafadhali tutumie kwa barua pepe: info@sikika.or.tz

Mgawanyo mbovu wa bajeti: Kikwazo katika utoaji wahuduma bora za afya

Na Gilbert Hapila

IMEBAINIKA kwamba mgawanyo wa bajeti ya sekta ya afya usiozingatia ukubwa wa maeneo, idadi ya watu na magonjwa husika ni kikwazo katika utoaji wa huduma bora za afya hapa nchini.

Zahati ya Iguguno katika Wilaya Iramba Mkoani Singida inayomilikiwa na kituo cha dini ikiwa ni moja ya kituo kinachotoa huduma bora za afya tofauti na zile zinazomilikiwa na Serikali mkoani humo.

Hali hii ilionekana katika ziara ya pamoja iliyofanywa na wadau wa maendeleo (Serikali, Asasi za Kiraia na Wafadhili) kama hatua ya maandalizi ya mkutano mkuu wa mwaka wa Sekta ya Afya (Joint Annual Health Sector Review (JAHSR), uliojadili halihalisi ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika sekta ya afya, vikwazo na vipaumbele vya mwaka 2012. Ziara hii ilifanyika mwezi Septemba mwaka 2011, katika wilaya kumi na mbili katika mikoa sita hapa nchini.

Katika ziara hiyo, Sikika ilipata fursa ya kutembelea wilaya mbili za Simanjiro mkoani Manyara na Iramba katika mkao wa Singida na kuweza kujionea hali halisi ya upatikanaji wa huduma za afya. Moja ya vitu vilivyobainika kwenye wilaya hizi mbili za Simanjiro na Iramba ni kwamba mgawanyo wa rasilimali fedha katika ngazi za halmashauri bado hauzingatii uwiano wa mahitaji.

Kijiografia wilaya za Simanjiro na Iramba ni kubwa zikiwa na mtawanyiko mkubwa wa watu ambo unahitaji bajeti kubwa ili kuweza kuhimili changamoto za usambazaji na usafirishaji wa dawa na vifaa tiba pamoja na watumishi wa afya kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali mbalimbali katika wilaya hizo. Hali hii pia ilielezewa na watumishi katika ngazi ya halmashauri (CHMT) kwamba inaathiri jitihada zao za kutembelea na kukagua vituo vyote vya afya kwani kwa kufanya hivyo seheme kubwa ya bajeti inaishia kwenye mafuta na fedha ya kujikimu. Kwa ujumla hali hii huathiri utoaji wa huduma za afya zenye ubora unaohitajika.

Tatizo hili la bajeti na kutozingatiwa mahitaji muhimu, kumechangia kwa kiasi kikubwa upungufu wa madawa na watumishi wa afya. Kwa mfano katika zahanati ya Iguguno wilayani Iramba, Sikika ilikuta daktari mmoja kati ya saba wanaohitajika akiwahudumia watu wengi na kujionea magodoro yasiyo na ubora ambayo hupatikana kwa bei rahisi.

Aidha, katika wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Sikika ilibaini tatizo kubwa la makazi kwa wahudumu wa afya ambao wanalazimika kuishi katika vibanda vya nyasi, ambavyo hutumiwa zaidi na wenyeji wa wilaya hiyo kama nyumba za kuishi, badala ya kujengewa nyumba zenye hadhi ya mtumishi wa afya ikiwa ni motisha kwa watumishi hao.

“Jambo la kushangaza ni kwamba hata katika vituo vya huduma ya afya ambavyo vina majengo ya kutosha kama vile kituo cha Afya cha Mererani, huduma za kulaza wagonjwa hazitolewi kutokana na idadi ya watumishi kuwa chini ikilinganishwa na miongozo ya wizara (staffing norms) pamoja na uhaba wa vitanda na magodoro” anasema Josaphat Mshighati Mratibu Kiongozi wa Programu katika shirika la Sikika.

Katika hatua nyingine Sikika ilibaini kuwa upo ushirikiswaji mdogo sana wa kamati za afya katika usimamizi wa huduma za afya, na hata pale ambapo wanahusishwa imekuwa ni kwa ajili ya kupitisha malipo ya tenda za ujenzi ama ukarabati wa majengo ya zahanati na vituo vya afya.

Kutokana na changamoto hizo ambazo zinasababisha kuwepo na utoji wa huduma mbovu za afya, Sikika ilitoa mapendekezo ambayo Serikali inatakiwa kuyazingatia ili kufanikisha mpango wa maboresho katika utoaji wa huduma za afya nchini.

Mapendekezo hayo ni bajeti yenye uwiano wa kimahitaji ikiwa ni pamoja na ukubwa wa eneo la wilaya husika. Mfano, Wilaya ya Simajiro pamoja na kwamba inahudumia wananchi wachache ikilinganishwa na wilaya ya Babati, bado inahitaji kutengewa bajeti kubwa kutokana na ukubwa wa eneo na changamoto za kijiografia. Hii itarahisisha usambazaji wa madawa na vifaa tiba katika vituo vyote vya huduma za afya na itatoa fursa za kutosha kwa ajili ya ukaguzi na usimamizi wa shughuli za maendeleo ya afya.

Mapendekezo mengine ni kuharakisha miradi ya kujenga makazi bora kwa watumishi wa sekta ya afya, kutoa motisha ya posho kwa watumishi wanaofanya kazi katika mazingira magumu, kujenga zahanati katika maeneo ambayo kuna uchache wa zahanati, na pia kuhakikisha kuwa kuna mgawanyo sawa wa watumishi wa sekta ya afya kati ya mijini na vijijini.

Wananchi kwa upande mwingine wanatakiwa kushiriki kwa makini katika vikao na mikutano inayohusu kujadili utoaji wa huduma za afya ili kuweza kutoa mapendekezo yatakayopelekea kuboresha huduma hizo.

Hivyo, Sikika inasisitiza Serikali itekeleze mpango wa kuongeza bajeti ya wizara ya afya hadi kufikia asilimia 15 kama ilivyo sainiwa katika azimio la Abuja 2001.

Wananchi wanapaswa kudai haki ya afya katika katiba ijayo ya Tanzania

Na Hope Lyimo

NI JUKUMU na wajibu wa kila taifa duniani kuboresha na kuhakikisha raia wake wako salama na kufanya kila liwezekanalo kuokoa maisha ya wananchi. Kwa maendeleo endelevu ya kila taifa ni wajibu wa nchi yeyote kuhakikisha kuwa raia wake wana afya njema ili kuweza kushiriki vyema kwenye maendeleo ya taifa ya jamii na pia ya kiuchumi.

Ili kuwa na afya bora, yampasa raia yoyote kupata huduma muhimu kwa maisha yake kama chakula, maji, malazi na huduma bora za afya, ambavyo ni muhimu kwa maisha yake ya kila siku. Katiba ya jamhuri ya muungano wa Tanzania inapaswa kujumuisha afya kama moja wapo ya haki muhimu za binadamu.Uwepo wa kipengele cha afya kwenye ibara za haki za binadamu kwenye katiba ya Tanzania kutapelekea wananchi kuweza kudai huduma bora za afya katika ngazi zote nchini.

Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo zimesaini mikataba ya kimataifa ambayo lengo lake ni kuboresha haki za afya duniani kote. Mkataba wa dunia wa haki za binadamu ambao Tanzania imesaini kushiriki katika maazimio hayo, katika ibara ya 25(1) inaelezea ifuatavyo:

“Kila mtu ana haki ya kuishi maisha ambayo yanampa uwezo wa kupata afya bora binafsi na ya familia yake, ikijumuisha lishe, malazi na huduma za afya na huduma bora za kijamii, na haki ya kupata usalama endapo hana ajira, maradhi, ulemavu, ujane, uzee ama matatizo ambayo yapo nje ya uwezo wake.”

Mwenyekiti wa Mchakato wa Katiba Tanzania Deusi Kibamba akitoa maelezo katika kongamano la mchakato wa katiba mpya.Huu ni muda muafaka kwa wananchi pia kuzungumzia masuala la afya kuwekwa katika mchakato huo.

Hivyo, Tanzania inapaswa kutekeleza makubaliano hayo kwa kujumuisha afya kama moja ya haki muhimu za binadamu kwa kila raia katika katiba ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ambavyo imeelezwa kwenye maazimio ya umoja wa mataifa. Hii itawezekana tu kama sisi ambao ni raia wa Tanzania tutaweza kuchukua jukumu la kujadili suala hili na kuitaka Serikali yetu kuhakikisha kuwa suala la afya bora linajumuishwa kwenye katiba mpya ya jamhuri ya muungano wa Tanzania kama moja wapo ya haki za msingi za binadamu.

Mfumo na huduma za afya Tanzania bado zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo mara nyingi husababishwa na uendeshaji mbovu, kutokuwajibika kwa walio madarakani na upungufu wa watoa huduma.Kujumuishwa kwa haki za afya kwenye katiba kutasaidia kwa namna moja au nyingine kwa wananchi kudai huduma bora za afya kwa mamlaka husika kwasababu raia watakuwa wanajua haki zao na wajibu wao.

Ni vyema sisi watanzania kwa ujumla wake tukajihusisha na mchakato wa kuunda katiba mpya ili hatimaye kuwe na katiba inayohakikisha watawala na watawaliwa wanatimiza majukumu yao ipasavyo katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwenye jamii. Ni jukumu la kila raia kutoa maoni yake katika mchakato wa uundwaji wa katiba mpya na kudai suala afya kujumuishwa kwenye kipengele cha haki za binadamu kama mojawapo ya haki za binadamu.

Motisha ni njia sahihi ya kuboresha huduma za afya nchini

Na Essau Mzuli

KUKOSEKANA kwa motisha na maslahi duni kwa watumishi wa sekta ya afya imegundulika kuwa ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili watoa huduma za afya hapa nchini.

Tatizo hilo kwa kiasi kikubwa limesababisha kuzorota kwa upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wailo wengi hasa wale wa kipato cha chini.

Kukosekana huko kwa motisha kwa watumishi wa afya kunachangia kuongezeka kwa uhaba wa watoa huduma za afya kwani watumishi wengine huacha fani ya uhudumu wa afya na kugeukia fani nyingine ambazo zina maslahi na motisha zaidi.

Katika nchi nyingi zinazoendelea ikiwemo Tanzania, watumishi wa sekta afya hufanya kazi katika mazingira magumu sambamba uhaba wa rasilimali muhimu kwa utoaji wa huduma za afya kama vile madawa,vifaa vya maabara,mafunzo na rasilimali watu pamoja na mapungufu ya kiutendaji kwa watendaji wakuu wa sekta ya afya nchini.

Hivyo, katika kutekeleza majukumu yake yenye lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watanzania wote, Sikika kupitia kitengo cha rasilimali watu imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali (kwa wapokea huduma na watoa huduma za afya) zenye lengo la kupata taarifa juu ya changamoto wanazokabiliana nazo katika kupokea na kupata huduma hizo.

Katika robo tatu ya mwaka 2011, kitengo Rasilimali watu katika sekta ya afya kilifanya utafiti ili kupata taarifa kutoka kwa watoa huduma za afya juu ya changamoto wanazokabiliana nazo katika kutoa huduma za afya. Utafiti huo ulifanyika katika wilaya sita ambazo ni Ilala, Kinondoni, Temeke (Dar es Salaam), Kibaha (Pwani) Kondoa na Mpwapwa (Dodoma).

Wauguzi wa Hospitali wakimshusha mgonjwa aliyekuwa amezidiwa kutoka kwenye gari la wagonjwa.Wauguzi hawa wanahitaji motisha ili kuweza kufanya kazi katika mazingira mzuri

Matokeo ya utafiti huo ambao ulihusisha watoa huduma za afya 44 yalidhihirisha wazi kwamba uwepo wa motisha kwa wafanyakazi wa afya kama vile mafunzo kazini na kupandishwa madaraja kwa wakati, mikopo ya fedha na vifaa vya ujenzi na thamani, kupewa nafasi za mafunzo ya muda mrefu na makazi bora ni njia muhimu za kuboresha huduma za afya nchini. Kwa mujibu wa utafiti huo, asilimia 70 ya watoa huduma za afya walidhihirisha kwamba kuongezwa kwa motisha kwa wafanyakazi ni njia madhubuti ambayo itawasukuma kufanya kazi kwa ari zaidi.

Kutokana na matokeo ya utafiti huo, Sikika inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Ofisi ya Rais kitengo cha menejimenti ya Utumishi wa Umma kuboresha mazingira ya utendaji wa kazi miongoni mwa watumishi wa afya nchini kwa kuwapa motisha. Pia inatoa wito kwa Serikali kuzingatia uanzishwaji na utekeleza motisha maalumu kwa watumishi wa afya wanaoishi maeneo ya vijijini ambao mazingira ya utendaji wa kazi ni magumu ukilinganisha na maeneo ya mjini.

Mhariri: Tuma Abdalla
Waandishi:
Victoria Amandus
Gilbert Hapila
Hope Lyimo
Essau Mzuli

P.O.Box 12183, Dar es Salaam
Tel: +255 222 666355/57, Fax: +255 222 6668015
Email: info@sikika.or.tz Website: www.sikika.or.tz